

# Majibu kuhusu Hekalu.

## Ndani ya hekalu kuko vipi?

Hekalu ni nyumba ya Bwana. Ni safi na nzuri ndani. Kila mmoja anavaa mavazi meupe na anajari-bu kuwa mnyenyeketu. Ni mahali pa amani pa kumwabudu Mungu, kujifunza na kuhisi upendo wa Mwokozi kupitia Roho Mtakatifu.



## Watu wanafanya nini ndani ya hekalu?

Ndani ya hekalu tunajifunza kuhusu mpango wa Mungu na kufanya **maagano** pamoja Naye. Tunafanya hivi kwa kushiriki katika **ibada** kama ubatizo, uthibitisho na kuunganishwa na familia zetu.



## "Nitavaaje ninapokwenda hekaluni?



Unapaswa kuvaan nguo zako nzuri kwenda hekaluni. Mara unapokuwa ndani, utabadi-lisha na kuvaan nguo maalumu ili kufanya ibada. Kwa ajili ya ubatizo, wafanyakazi wa hekaluni watakupa vazi jeupe la kuvaan.

## Inamaanisha nini kufanya ubatizo kwa niaba ya wafu?

Ndani ya hekalu, unaweza kubatizwa kwa niaba ya watu waliokufa bila kubatizwa. Utavaa mavazi meupe na kuzamishwa ndani (pasipo chochote kubaki juu) ya maji



## Kibali cha hekaluni ni nini?

Kibali cha hekaluni ni kipande kidogo cha karatasi amba-cho kinakuruhusu wewe kuingia heka-luni. Unaweza kuki-pata kutoka kwa mshiriki wa uaskofu wako au urais wa tawi. Atakuuliza kama unatii amri na kama una ushuhuda. Kama unastahili na uko tayari kui-ningia hekaluni, atakupa kibali cha hekaluni.



## NINI MAANA YA IBADA YA UKUHANI?

Ibada ya ukhansi ni tendo takatifu ambalo linafanya kwa mamlaka na nguvu kutoka kwa Mungu. Ubatizo, uthibitisho na sakramenti ni ibada ambazo hufanyika nje ya hekalu. Ubatizo wa hekaluni, endaumenti na kuunganishwa ni ibada ambazo hufanyika ndani ya hekalu.



## BABA WA MBINGUNI



## AGANO NI NINI?

Agano ni ahadi ya pande mbili tunayofanya na Baba wa Mbinguni. Tunamuahidi Yeye vitu fulani, na Yeye anaahidi kuwa pamoja nasi na kutubariki.